

Jiunge na Mpango wa Jaribio wa Ada za Usafiri Zilizopunguzwa wa Kaunti ya Allegheny!

Idara ya Huduma za Binadamu (DHS, Department of Human Services) ya Kaunti ya Allegheny inatafuta wapokeaji wa msaada wa Mpango wa Msaada wa Chakula cha Ziada (SNAP, Supplemental Nutrition Assistance Program) wenye umri wa miaka 18 hadi 64 ili kushiriki kwenye mpango wa jaribio wa miezi 12 ili kuelewa athari ya uwezo wa kumudu usafiri kwa wakazi wenye mapato ya chini.

Ni nani anayestahiki kushiriki kwenye Mpango wa Jaribio wa Ada za Usafiri Zilizopunguzwa wa Kaunti ya Allegheny?

Washiriki wanaostahiki:



Wanaoishi kwa sasa katika Kaunti ya Allegheny



Waliokuwa wanapokea msaada wa SNAP kufikia tarehe 30 Septemba 2022



Walio na umri wa kati ya miaka 18 na 64



Wasio na mwanafamilia mwingine mwenye umri wa miaka 18 hadi 64 ambaye tayari anashiriki kwenye mpango huu wa jaribio

Mpango huu wa jaribio unafanyaje kazi?

Ni hiari ya mtu kushiriki kwenye mpango wa jaribio lakini inajumuisha kukubali na kushiriki data na kujaza utafiti wa mara kwa mara. Washiriki wanaostahiki watawekwa kwenye mojawapo ya makundi matatu bila mpangilio maalum:

1

Usafiri wa bure: Kikundi hiki kitasafiri bure bila kikomo kwenye safari zote za PRT kwa miezi 12.

2

Punguzo la asilimia 50: Kikundi hiki kitapewa ConnectCard ambayo inapunguza nusu (50%) ya gharama ya safari zote za PRT kwa miezi 12, na tayari ina mjazo wa \$10.

3

Hakuna punguzo: Kikundi hiki kitapewa ConnectCard ambayo tayari ina mjazo wa \$10 lakini hakitapewa punguzo la ada ya usafiri.

Kwa nini ni mpango wa jaribio badala ya kuwa mpango wa kudumu?

Mpango wa jaribio ni fursa ya muda mfupi ya kupata maoni ya washiriki kwa lengo la kupata maarifa ya kubuni mpango wa kudumu.

DHS ingependa kuelewa jinsi wakazi wa eneo wanavyoweza kufaidika kutokana na kupunguzwa kwa gharama ya usafiri wa umma. Hii itajumuisha kuchunguza athari ya kusafiri kwa kutumia gari moja na iwapo kuna ongezeko la upatikanaji wa kazi, huduma na mahitaji mengine ya wakazi.



Ili kupata maelezo zaidi na kutuma maombi, tembelea: DiscountedFares.alleghenycounty.us



Allegheny County
Discounted Fares
Pilot Program

